

# **Ikimbieni Zinaa**

**na**

**Ellis P. Forsman**

# **Ikimbieni Zinaa**

**na**

**Ellis P. Forsman**

**Oktoba 11, 2011**

# **Ikimbieni Zinaa**

## **1 Kor. 6:18**

Wakristo wa kule Korintho walikumbana na changamoto kuu katika kuishi maisha matakatifu.

Mji huo ulikuwa umejulikana kwa ujisadi. Hekalu la Venus ulichukua makuhani wa kike waliojitoa takriban 1000 katika ukahaba wakitumia jina la dini.

Baadhi ya Wakristo waliacha ujisadi kutokana na uongofu wao. 1 Kor. 6:9-11, “*Au hamjui ya kuwa wadhalimu hawatauridhi ufalme wa Mungu? Msidanganyike; waasherati hawataurithi ufalme wa Mungu, wala waabudu sanamu, wala wazinzi, wala wafiraji, wala walawiti, wala uevi, wala watamano, wala watukanaji, wala wanyang’anyi. Na baadhi yenu mlikuwa watu wa namna hii; lakini mlioshwa, lakini militakaswa, lakini mlihesabiwa haki katika jina la Bwana Yesu Kristo, na katika Roho wa Mungu wetu.*”

Na Paulo anawaonya “Kukimbia zinaa”. 1 Kor. 6:18, “*Ikimbieni zinaa. Kila dhambi aitendayo mwanadamu ni nje ya mwili wake; ila ye ye afanyakaye zinaa hutenda dhambi juu ya mwili wake mwenyewe.*”

Wito huo unahitajika leo pia. Ujisadi (Uzinzi) ni mwangi katika mila zetu. Zinaa inatafsiriwa (na kutokutafsiriwa), ikiwasababisha wengine kujiingiza katika tabia ya hatari.

Wale wanaomfuata Kristo lazima wawe na uelewa mzuri wa kile ambacho ni kibaya. Na hivi leo watu wanahitaji kuonywa, “Kuikimbia zinaal!”

Kwa sababu wengi wanatafsiri vibaya ujisadi leo, tunafanya vizuri kwa tahadhari ya kwanza tafsiri ya Biblia kuhusu tabia hipi ambayo tunatakiwa kuikimbia.

## **Tafsiri ya zinaa**

### **Maneno ya jumla.**

Neno la Kiyunani imetafsiri neno zinaa (KJV), tabia ya uzinzi (NKJV) ni porneia.

“Kiujumla inatumika kuonyesha dhambi ye yote ya uzinzi” – Kamusi ya maneno yaliyotafsiriwa.

Hivyo inajumuisha tendo “lolote la uzinzi: Uasherati, uzinzi, usodoma, kushiriki uzinzi na wanyama, n.k.” – Thayer.

## **Maneno ya Wazi.**

**Wazinzi** (moichao) – kushirikiana kimwili kinyume cha sheria na mwenza wa mwingine – Thayer

**Usodoma** (arsenokoites) – mtu anayelala na mwanaume mwezake kama kwa mwanamke, tendo la ndoa la jinsia moja.

- 1 Kor. 6:9, “*Au hamjui ya kuwa wadhalimu hawataurithi ufalme wa Mungu? Msidanganyike; waasherati hawataurithi ufalme wa Mungu, wala waabudu sanamu, wala wazinzi, wala wafiraji, wala walawiti.*”
- 1 Tim. 1:10, “*Na wazinifu, na wafiraji, na waibao watu, na waongo, nao waapao kwa uongo; na likiwapo neno lo lote lingine lisilopatana na mafundisho yenyе uzima;*”

**Kuzini na wanyama** – kulala na wanyama. Walawi 18:23, “*Wala usilale na mnyama ye yote, ili kujitia unajisi kwake; wala mwanamke asisimame mbele ya mnyama ili kulala naye; ni uchafuko.*”

**Uchafu** – (aselgia) – uchafu, uharibifu, kuzini kupita kiasi, hamu isiyo ya kawaida, - Kamusi Iliyokamilika. Rum. 13:13, “*Kama ilivyhusika na mchana na tuenende kwa adabu; si kwa ulafi na ulevi, si kwa ujisadi na uasherati, si kwa ugomvi na wivu.*” Neno hili linaweza kujumlisha tendo la ndoa la mdomo, ambayo wengine wamejaribu kutafsiri kwamba siyo ngono, ambayo pia imekuwa tatizo kubwa mionganoni mwa vijana (na madhara yanayotisha).

**Uzinzi** – ni neno la jumla la tendo la ndoa. Zinaa ni uzinzi; lakini uzinzi ni neno pana ambayo inajumuisha dhambi zingine za uzinzi pia.

Marufuku dhidi ya uzinzi inaweza kushukuriwa tu pale tunapoelewa...

## **Maangamizi ya uzinzi**

### **Inaangamiza mwili.**

Magonjwa mengi ya bacteria mara nyingi huletwa kwa sababu ya uzinzi. Mengi ya magonjwa haya yaletwayo na uzinzi hayatibiki. Watu wengi wamajifunza njia ngumu, kitu ambacho Solomoni aliwaonya watu wake. Mithali 5:11-12, “*Nawe ukaziombolea siku zako za mwisho, nyama yako ya mwili wako utakapoangamia; ukasema jinsi nilivyochochukia maonyo, na moyo wangu ukadharau kukemewa,*”

## Inaangamiza mji.

Ndoa iliyodhamiriwa kukaa maisha yote uvunjika, maranyingi haiwezi kurekebishwa. Math. 19:4-6, “*Akajibu akawaambia hamkusoma ya kuwa yeye aliyewaumba mwanzo, aliwaumba mtu mume na mtu mke, akasema, kwa sababu hiyo, mtu atamwacha babaye na mamaye, ataambatana na mkewe; na hao wawili watakuwa mwili mmoja? Hata wamekuwa si wawili tena, bali mwili mmoja. Basi aliowaunganisha Mungu mwanaadamu asiwatenganishe.*”

Watoto wanaangamizwa, kwa madhara ya hisia ambayo huenda hadi ukubwani. Mal. 2:16, “*Maana mimi nakuchukia kuachana, asema BWANA, Mungu wa Israeli; naye aifunikizaye nguo yake kwa udhalimu namchukia asema BWANA wa majeshi; basi jihadharini roho zenu, msije mkatenda kwa hiana.*”

Sehemu ya ndoa ijayo inawekwa chini (ni nani anayenda “mema yaliyo haribiwa” kwa sababu ya magonjwa?).

## Inaangamiza nafsi.

Itakuwa vigumu kujisamehe mwenyewe, kutakuwa na kujilaumu binafsi. Mithali 5:12-13, “*Ukasema, jinsi niliwyochukia maonyo, na moyo wangu ukadharau kukemewa; wala sikuisikia sauti ya waalimu wangu, wala sikuwategeea sikio langu walionifundisha!*”

Nafsi yako itanyimwa marafiki wazuri, ambao uliharibu uaminfu wao. Mithali 6:30-35, “*Watu hawamdharaau mwivi, akiiba ili kujishibisha, iwapo aona njaa; lakini akipatikana atalipa mara saba; atatoa mali yote ya nyumba yake. Mtu aziniye na mwanamke hana akili kabisa; afanya jambo litakalomiwangamiza nafsi yake. Atapata jeraha na kuvunjiwa heshima; wala fedheha yake haitafutika. Maana vivu ni ghadhabu ya mtu; wala hatahurumia siku ya kujilipiza kisasi. Hataku bali ukombozi uwao wote; wala hatakuwa radhi, ujapomlipa vitu vingi.*”

Kama nilitubu na sikusamehewa, hakuna tumaini.

- 1 Kor. 6:9-10, “*Au hamjui ya kuwa wadhalimu hawataurithi ufalme wa Mungu? Msidanganyike; waasherati hawataurithi ufalme wa Mungu, wala waabudu sanamu, wala wazinzi, wala wafiraji, wala walawiti, wala wevi, wala watamario, wala walevi, wala watukanaji, wala wanyang’anyi.*”
- Gal. 5:19-21, “*Basi matendo ya mwili ni dhahairi, ndiyo haya, uasherati, uchafu, ujisadi, ibada ya sanamu, uchawi, uadui, ugomvi, vivu, hasira, fitina, faraka, uzushi, husuda, ulevi, ulafi, na mambo yanayofanana na hayo, katika hayo nawaambia mapema,*

*kama nilivyokwisha kuwaambia ya kwamba watu watendao mambo ya jinsi hiyo hawataurithi ufalme wa Mungu.”*

- Ebr. 13:4, “*Ndoa na ieshimiwe na watu wote, na malazi yawe safi; kwa maana waasherati na wazinzi Mungu atawahukumia adhabu.”*

Tunaona ni kwa nini Paulo anaandika “*Ikimbie zinaa*”. Haipaswi kuchukuliwa kirahisi! Ili kwamba tuweze kufanikiwa kwa kuikimbia zinaa, hapa kuna baadhi ya mawazo juu ya...

## **Madhara ya Uzinzi**

### **Jifunze kwa Yusufu.**

Alikuwa amefaulu kwa kuikimbia uzinzi kwa mke wa Potifa. Mwanzo 39:7-12, “*Ikawa baada ya mambo hayo, mke wa bwana wake akamtamani Yusufu, akamwambia lala nami. Lakini akakataa, akamwambia mke wa bwana wake, tazama bwana wangu hajui kitu kilichowekwa kwangu nyumbani, na vyote alivyo navyo amevititia mkononi mwangu. Hakuna mkuu katika nyumba hii kuliko mimi, wala hakunizulia kitu chochote ila wewe, kwa kuwa wewe u mkewe. Nifanyeje ubaya huu mkubwa nikamkose Mungu? Akawa akizidi kusema na Yusufu siku baada ya siku, lakini hakumsikia alale naye, wala aongee naye. Ikawa siku moja akaingia nyumabni atende kazi yake, wala hapakuwa na mtu katika watu wa nyumbani humo ndani; huyo mwanamke akamshika nguo zake, akisema, lala nami. Yusufu akaiacha nguo yake mkononi mwake, akakimbia akatoka nje.*”

Cha muhimu zaidi, alithamini uhusiano wake na Mungu. Mwanzo 39:9, “*Hakuna mkuu katika nyumba hii kuliko mimi, wala hakunizulia kitu chochote ila wewe, kwa kuwa wewe u mkewe. Nifanyeje ubaya huu mkubwa nimkose Mungu?*”

Hivyo kimbia tamaa za ujanani, badala yake uweke uungu. 2 Tim. 2:22, “*Lakini zikimbie tama za ujanani ukafuate haki, na imani, na upendo, na amani, pamoja na wale wamwitao Bwana kwa moyo safi.*”

### **Jifunze kwa Solomoni.**

Alimwonya mwanaye kuhusu mushahara wa uzinzi.

- Mith. 5:1-6, “*Mwanangu sikiliza hekima yangu; tega sikio lako; mzishike akilizangu; upate kuilinda busara, na midomo yako iyahifadhi maarifa. Maana midomo ya Malaya hudondosha asali, na kinywa chake ni laini kuliko mafuta; lakini mwisho wake ni mchungu kuliko pakanga; ni mkali kama upanga wa makali kuwili. Miguu yake inatelemkia mauti, hatua zake zinashikamana na*

*kuzimu, hata asiweze kuiona njia sawa ya uzima; njia zake ni za kutanga – tanga wala hana habari.”*

- Mith. 5: 9-14, “*Usije ukawapa wengine hekima yako, na wakorofii miaka yako; wageni wasije wakashiba nguvu zako; kazi zako zikawa ndani ya nyumba ya mgeni naue ukazionbolea siku zako za mwisho, nyama yako ya mwili wako utakapoangamia; ukasema jinsi nilivyochukia maonyo, na moyo wangu ukadharau kukemewa; wala sikuisikia sauti ya waalimu wangu, wala sikuwategea sikio langu walionifundisha! Nalikuwa karibu kuingia katika maovu yote, katikati ya m Kutano na kusanyiko.*”
- Mith. 5:20-23, “*Mwanangu! Mbona unashangilia Malaya, na kukikumbatia kifua cha mgeni? Kwa maana njia za mwanadamu zi mbele ya macho ya BWANA na mienendo yake yote huitafakari. Maovu yake ye ye yatampata mdhalimu, naye atashikwa kwa kamba za dhambi zake. Atakuza huyo kwa kukosa maonyo, naye atapotea kwa wingi wa ujingga wake.*”

Aliye washauri wanawe kuepukana na mtu mzinzi.

- Mith. 5:7-8, “*Basi, wanangu, nisikilizeni sasa, wala msiache maneno ya kinywa changu. Itenge njia yako mbali naye, wala usiukaribie mlango wa nyumba yake.*”
- Mith. 7:24-27, “*Basi, wanangu, nisikilizeni sasa, mkayaangalie maneno ya kinywa changu. Moyo wako usizielekee njia zake, wala usipotee katika mapito yake. Maana amewaangusha wengi waliojeruhiwa, naam, jumla ya waliouawa naye ni jeshi kubwa. Nyumba yake ni njia ya kwenda kuzimu, hushuka mpaka nyumba ya mauti.*”

Aliyemtia mwanaye moyo kupenda mke wa ujana wake.

- Mith. 5:20, “*Mwanangu mbona unashangilia Malaya, na kukikumbatia kifua cha mgeni?*”
- Mith. 5:18, “*Chemchemi yako ibarikiwe; naue umfurahie mke wa ujana wako.*”
- Mhu. 9:9, “*Uishi kwa furaha pamoja na mke umeppendaye, siku zote za maisha yako ya ubatili, ulizopewa chini ya ju; siku zote za ubatili wako, kwa maana huu ni sehemu yako ya maisha; na katika taabu zako ulizozitaabika chini ya juu.*”

## Jifunze kupitia Daudi.

Ambae alifanya kosa mbaya na Bethsheba. 2 Sam. 11:3-5, “*Naye Daudi akapeleka akauliza habari za yule mwanamke. Mtu mmoja akasema, je! Huyu siye Bath – sheba, binti Eliamu, mkewe Uria, Mhiti? Basi Daudi akapeleka wajumbe, akamtwa; naye akaingia kwake; naye akalala naye; maana yule mwanamke amekwisha kutakasika unajisi wake; kisha akarudi nyumbani kwake. Yule mwanamke akachukua mamba; basi akapeleka na kumwambia Daudi akasema, ni mjamzito.*”

Ambayo ilipelekea kifo cha Uria, na kifo cha motto.

- 2 Sam. 2:6-17, “*BWANA naye sasa awatendee ninyi fadhili na kweli, mimi nami nitawalipeni fadhili hiyo, kwa sababu mmetenda jambo hilo. Basi sasa mikono yenu na itiwe nguvu, nanyi iweni mashujaa; maana Sauli bwana wenu amekufa tena nyumba ya Yuda wamenitia mimi mafuta niwe mfalme juu yao. Basi Abneri, mwana wa Neri, amiri wa jeshi la Sauli, alikuwa amemtwaa Ishboseth, mwana wa Sauli, na kumvusha na kumpeleka mahanimu; akamweka awe mfalme juu ya Gileadi, na Waasherri, na Yezreeli, na Efraimu, na Benyamin, na juu ya Israeli wote. Huyo Ishbpsethi, mwana wa Sauli, umri wake ulikuwa amepata miaka arbaini alipoanza kutawala juu ya Israeli, akatawala miaka miwili. Lakini nyumba ya Yuda waliandamana na Daudi. Na wakati Daudi alipotawala Hebronii juu ya nyumba ya Yuda ulikuwa miaka saba na miezi sita. Basi Abneri mwana wa Neri, na watumishi wa Ishbosethi, mwana wa Sauli, wakatoka Mahanimu kwenda Gibeoni. Huyo Yoabu naye mwana wa Seruya, na watumishi wa Daudi, wakatoka wakakutana nao karibu na ziwa la Gibeoni; wakaketia hawa upande huu wa ziwa, na hawa upande huu wa ziwa. Abneri akamwambia Yoabu, tafadhalii vijana hawa na waondoke na kucheza mbele yetu. Yoabu akasema, haya na waondoke. Basi wakaondoka wakaenda upande wa pili kwa hesabu yao watu kumi na wauili wa Benyamini, na wa Ishboseth, mwana wa Sauli na watu kumi na wauili wa watumishi wa Daudi. Wakakamatana, kila mtu akimshika mwenziwe kichwa chake, na kutia upanga wake katika ubavu wa mwenzake; wakaanguka pamoja hata mahali pale pakaitwa Helkath – hasurimi, napo ni katika Gibeoni. Vita vile vilikuwa vikali sana siku ile; naye Abneri akashindwa na watu wa Israeli, mbele ya watumishi wa Daudi.*”
- 2 Sam. 12:9-19, “*Kwa nini umelidharau neno la BWANA na kufanya yaliyo mabaya machoni pake? Umempiga Uria, Mhiti kwa upanga, naue umemtwaa mkewe awe mke wako, naue umemuuwa huyo kwa upanga wa wana wa Amoni. Basi sasa*

*upanga hautaondoka nyumbani mwako, kwa sababu umenidharau, ukamtwaan mkewe Uria, Mhiti, kuwa mke wako. BWANA asema hivi, angalia nitakuondokeshea uovu katika nyumba yako, nami nitawatwaa wake zako mbele ya macho yako, na kumpa jirani yako, naye atalala na wake zako mbele ya jua hili. Maana wewe ulifanya jambo hili kwa siri; bali mimi nitalifanya jambo hili mbele ya Israeli wote na mbele ya jua. Daudi akamwambia Nathani, nimemfanyia BWANA dhambi. Nathani akamwambia Daudi, BWANA naye ameiondoa dhambi yako; hutakufa. Lakini, kwa kuwa kwa tendo hili umewapa adui za BWANA nafasi kubwa ya kukufuru, mtoto atakayezaliwa kwako hakika naye atakufa. Naye Nathani akaondoka kwenda nyumbani kwake. Basi BWANA akampiga yule mtoto ambaye mkewe Uria alimzalia Daudi naye akawa hawezi sana. Basi Daudi alimwombwa Mungu kwa ajili ya mtoto, Daudi akafunga, akaingia akalala usiku kucha chini. Nao wazee wa nyumba yake wakaondoka, wakasimama karibu naye, ili wamuwinue katika nchi; lakini hakukubali, wala hakula chakula pamoja nao.”*

Lakini Daudi alikiri dhambi zake, na kutubu.

- 2 Sam. 12:13, “Daudi akamwambia Nathani, nimemfanyia BWANA dhambi. Nathani akamwambia Daudi, BWANA naye ameiondoa dhambia yako; hutakufa.”
- Zaburi 51:1-4, “Ee Mungu unirehemu, sawasawa na fadhili zako. Kiasi cha wingi wa rehema zako, uyafulute makosa yangu. Unioshe kabisa na uovu wangu, unitakase dhambi zangu. Maana nimejua mimi makosa yangu na dhambi yangu I mbele yangu daima. Nimekutenda dhambi wewe peke yako, na kufanya maovu mbele za macho yako. Wewe ujulikane kuwa una haki unenapo, na kuwa safi utoapo hukumu.”

## Hitimisho

Kukimbia uzinzi na madhara yake mabaya...

- Tunatakiwa kuwa na tabia ya Yusufu, na kutumia hekima ya Sulemani.
- Inapo kuwa muhimu, tunaitaji toba ya Daudi.

Lazima tusichukue uzinzi kirahisi.

Inaweza kuangamiza mwili wako, mji, na nafsi. Msamaha unawezekana, lakini madhara ya kimwili ya dhambi mara nyingi hubaki (magonjwa).

1 Kor. 6:11, “Na baadhi yenu mlikuwa watu wa namna hii; lakini mlioshwa, lakini mlitakaswa, lakini mlihesabiwa haki katika jina la Bwana Yesu Kristo, na katika Roho wa Mungu wetu.”

Hivyo, ikimbie zinaa, na uache kufanya ngono, ambayo ndiyo mapenzi ya Mungu kwako. 1 Wathes. 4:1-8, “Iliyobaki ndugu tunakusihini na kuwaonya ya kwamba mwenende katika Bwana Yesu; kama mlivyopokea kwetu sisi iwapasavyo kuenenda na kumpenda Mungu, kama nanyi mnavyoenenda, vivyo hivyo mpate kuzidi sana. Kwa kuwa mnajua ni maagizo gain tuliyowapa kwa Bwana Yesu. Maana haya ndiyo mapenzi ya Mungu, kutakaswa kwenu, muepukane na uasherati; kila mmoja wenu ajue kuuweza mwili wake katika utakatifu na heshima; si katika hali ya tama mbaya, kama mataifa wasiomjua Mungu. Mtu asimpunje ndugu yake wala kumkosa katika jambo hili; kwa kuwa Bwana ndiye alipizaye kisasi cha haya yote; kama tulivyowaambia kwanza tukashuhudia sana. Maana Mungu hakutuitia uchafu, bali tuwe katika utakaso. Basi yeche anayekataa, hakatai mwanadamu bali Mungu, anayewapa ninyi Roho wake Mtakatifu.”



